

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA**

**23 MEI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA – TAREHE 23 MEI, 2023

#### I. DUA:

#### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

#### WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

#### III. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 401. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini barabara ya Mombo Mzeri itajengwa kwa kiwango cha lami.

**402. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Kituo cha Afya cha Msanda Muungano katika Tarafa ya Mpui.

**403. MHESHIMIWA CHARLES JOHN MWIJAGE (MULEBA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Serikali isikae na Taasisi za Afya za Kidini Wilayani Muleba ili kupunguza changamoto zilizopo katika kutoa huduma.

**WIZARA YA AFYA:**

**404. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya;-

Je, upi mkakati wa kutokomeza wizi wa dawa na vifaa vya afya, hatua zilizochukuliwa kwa wahusika na fedha zinazopotea kwa mwaka.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **405. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la umeme Mkoani Mtwara hususani Wilaya ya Masasi na Jimbo la Lulindi.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **406. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):**

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati na kuongeza uwezo wa Gereza la Dimani Wilayani Kibiti.

### **407. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Mlima Nkongore utarudishwa kwa Wananchi wa Kata ya Katare baada ya kuchukuliwa na Jeshi la Magereza.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **408. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Kijiji cha Kalema Maziwani linalounganisha Wilaya za Kiteto, Chemba na Kondo.

### **409. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba kwa kiwango cha lami.

### **410. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kwa nini Serikali haijazikarabati Meli za Mv. Liemba, Mv. Mwongozo na Mv. Sangara ambazo zimesimama kufanya kazi.

**WIZARA YA MAJI:**

**411. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA  
(NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka maji katika Vijiji 62 Jimbo la Newala Vijijini ambavyo havina huduma ya maji.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**412. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za kimkakati kufikia usawa wa kijinsia 50/50 ifikapo 2025.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**413. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kwa nini ukomo wa saa za kufundisha Wanafunzi haujawekwa kisheria kama ilivyowekwa kwa saa za kazi kwa Waajiriwa.

**WIZARA YA KILIMO:**

**414. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI  
MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaongeza eneo na kuboresha Skimu ya Umwagiliaji ya Mto Ruvu - Bagamoyo.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
23 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**